MKUTANO WA SITA

KIKAO CHA KWANZA - TAREHE 29 JANUARI, 2002

Kikao kitaanza saa Tatu Asubuhi
na Dua Zitasomwa

I. KIAPO CHA UAMINIFU

Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed

II. TAARIFA YA SPIKA

III. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

WAZIRI MKUU:

Nakala za matoleo yote ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake zilizochapishwa tangu Kikao cha Mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita.

WAZIRI WA FEDHA:

Taarifa ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Hesabu za Miji na Wilaya kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 31 Desemba, 2000 (Report of the Controller and Auditor-General on Local Authority Accounts for the Year ended 31st December, 2000).

IV. MASWALI

OFISI YA WAZIRI MKUU:

1. MHESHIMIWA MARIAM SALUM MFAKI (VITI MAALUM): Atamwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu: Kwa kuwa Madhumuni ya uanzishwaji wa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma (CDA), yalikuwa ni kuandaa mazingira mazuri ya kuwahamishia Viongozi na Watumishi wa Wizara mbalimbali kwenye Makao Makuu ya Serikali Dodoma; na kwa kuwa kulikuwa na miradi iliyoainishwa kutekelezwa na Mamlaka hiyo:

(a) Je, ni miradi gani iliyopangwa kutekelezwa na Mamlaka hiyo na ni miradi gani imekwisha tekelezwa hadi sasa;

(b) Je, Mamlaka hiyo ilipewa muda gani wa kutekeleza miradi hiyo;

(c) Je, ni kwa nini mamlaka hiyo haizitengenezi barabara za lami za Manispaa ya Dodoma ambazo zinaonekana kujaa vumbi na hazilingani na barabara za Manispaa nyingine kama vile Arusha, Iringa, Ilala, Kinondoni n.k.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

2. MHESHIMIWA MAKANGA (BARIADI MASHARIKI): Atamwuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi: Kwa Kuwa zoezi la ukaguzi wa magari (Vehicle Inspection) hufanyika kila mwaka, yaani Wiki ya Nenda Kwa Usalama, na kwa kuwa lengo kuu la ukaguzi huo ni kuhakikisha kuwa magari yote yako salama kwa matumizi barabarani (Road Worthy) na kupewa vitambulisho (stickers) baada ya kulipia ukaguzi huo:

(a) Je, kuanzia mwaka 1995 hadi sasa ni magari mangapi yalikaguliwa na ni kiasi gani cha fedha kilipatikana kutokana na zoezi hilo;

(b) Kwa kawaida fedha zozote zinazokusanywa na Serikali hutolewa stakabadhi (ERV) lakini katika zoezi hilo ERV huwa hazitolewi, na badala yake hutolewa "stickers"; Je, ni kwa nini hufanyika hivyo;

(c) Je, wananchi watahakikishaje kuwa fedha hizo zinaingia kwenye mfuko wa Serikali.

3. MHESHIMIWA YAHYA KASSIM ISSA (CHWAKA): Atamwuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi: Kwa kuwa Bunge ni chombo cha juu cha Serikali

ambacho hukutana kwa vipindi vinne (4) kwa kila mwaka ili kupanga na kutekeleza majukumu yake; na kwa kuwa hivi sasa ugaidi umepamba moto kwa baadhi ya nchi hadi kufikia hapa Tanzania katika Ubalozi wa Marekani:

(a) Je, Serikali inawaeleza nini Wajumbe waliomo ndani ya chombo cha Bunge kwa uhakika wa usalama wa maisha yao;

(b) Je, Serikali kwa nyakati za Vikao vya Bunge haioni kwamba iko haja ya kuchukua hatua za tahadhari za Ulinzi wa dhahiri badala ya huu uliopo.

WIZARA YA UJENZI:

4. MHESHIMIWA MAJOR MAKUNDI (VUNJO): Atamwuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi: Kwa kuwa Serikali ilipojibu Swali Na. 33 katika Mkutano wa Tatu wa Bunge tarehe za Machi, 2001 ilieleza kuhusu ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Marangu-Mwika-Rombo na ile ya Himo-Kilacha-Mwika-Rombo-Kamwanga mpakani mwa Kenya na Tanzania kwa ajili ya usafirishaji wa mazao kati ya nchi hizo mbili:

(a) Je, utekelezaji wake umefikia wapi;

(b) Je, ni Mkandarasi gani anayefanya kazi hiyo na itakamilika lini.

5. MHESHIMIWA MUSALIKA (NYANG'WALE): Atamwuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi: Kwa kuwa katika mwaka wa Fedha wa 1999/2000 Serikali ilitoa fedha za kujenga daraja la Wingi lililoko mpakani mwa Wilaya ya Sengerema na Geita pamoja na kunyanyua tuta katika mbuga ya Nyang'holongo na kujenga makaravati matatu sehemu hiyo katika barabara ya Busisi hadi Nyang'holongo; na kwa kuwa mvua za msimu wa 2000/2001 zilipelekea kuharibika kwa sehemu hiyo ya barabara kwa sababu ilikuwa haijakamilika kujengwa:

(a) Je, ni lini Serikali itamalizia ujenzi wa sehemu hiyo kwa kiwango kinachohitajika;

(b) Je, Serikali haijui kuwa umefika wakati wa kutenga fedha za kutosha kujenga barabara hiyo muhimu inayounganisha Wilaya za Sengerema, Geita na Kahama na inayoanzia Busisi kupitia Buyagu, Ngoma, Busolwa, Nyang'hwale, Nyijundu, Karumwa, Bukwimba hadi Nyang'holongo.

WIZARA YA AFYA:

6. MHESHIMIWA MLOKA (MOROGORO MJINI): Atamwuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya: Kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tatu iko makini sana katika utekelezaji wa majukumu yake; na kwa kuwa nchini mwetu ipo dawa ya unga inayotokana na miti shamba inayodaiwa kutibu magonjwa zaidi ya 120 inayojulikana kwa jina la NGETWA ambayo tayari imeshasambazwa katika maduka mengi ya madawa:

(a) Je, Serikali inatoa tamko gani kwa wananchi wake kuhusu ukweli wa tiba hiyo;

(b) Je, kuna athari/madhara yoyote kwa mtumiaji hasa ikizingatiwa kutokuwepo kipimo sahihi cha matumizi ya dawa hiyo.

7. MHESHIMIWA NYAWAZWA (VITI MAALUM): Atamwuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya: Kwa kuwa Wakunga wengi hususani wa Kata ya Bukanda Wilaya ya Ukerewe na sehemu nyingi za Vijijini husaidia sana akina mama wajawazito na watoto baada ya Saa 9.30 mchana, muda ambao ni wa kawaida kwa saa za kazi za Serikali:

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kutamka wazi kuwa Wakunga Vijijini watambulike katika Taifa letu kwa kazi nzuri ya kuokoa maisha ya Wanawake wajawazito Vijijini;

(b) Je, Serikali haioni haja ya kuwapa kipaumbele katika kutoa kinga za maradhi ya kuambukiza wakati wakitoa huduma hizo;

(c) Je, Serikali haiwezi kutoa mafunzo au semina kwa Wakunga hao ili nao wapate motisha ya elimu katika kazi yao wanayoifanya.

WIZARA YA KILIMO NA CHAKULA:

8. MHESHIMIWA MUSSATI (KASULU MASHARIKI): Atamwuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula: Kwa kuwa katika miaka ya 1980 Serikali ilianzisha mradi wa umwagiliaji maji katika bonde kubwa lililopo katika Kijiji cha Titye kwenye Jimbo la Kasulu Mashariki lakini haukukamilika:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuukamilisha mradi huo;

(b) Je, kuna mpango gani wa kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika Mabonde makubwa na mazuri yaliyoko kwenye Vijiji vya Rungwe Mpya, Kanazi na Buhoro Jimboni Kasulu Mashariki;

9. MHESHIMIWA BUZUKA (SOLWA): Atamwuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula: Kwa kuwa Wizara mpya ya Kilimo na Chakula pamoja na majukumu yake mengine inakusudia kuchochea kilimo bora na cha kisasa na hasa kilimo cha umwagiliaji maji;

Je, Serikali imejiandaaje kutumia maji ya Ziwa Victoria katika kilimo cha umwagiliaji ili kuinua uzalishaji wa chakula na kupambana na janga la njaa la mara kwa mara ambalo hulileta fedheha Taifa letu.

WIZARA YA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:

10. MHESHIMIWA KIGWALILO (LIWALE): Atamwuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: Kwa kuwa mawasiliano ya simu ni kichocheo kikubwa cha maendeleo kwa kuongeza ufanisi katika shughuli mbalimbali za Kiserikali, Kijamii na Kibiashara; na kwa kuwa Serikali inaelewa kwamba Wilaya ya Liwale haina mawasiliano ya simu kwa muda mrefu:

    (a) Je, Serikali ina mpango gani wa uhakika wa kuipatia Wilaya ya Liwale mawasiliano ya simu kama ilivyo kwenye Wilaya nyingine;

    (b) Je, Serikali haioni kwamba kuendelea kutowapatia wananchi wa Wilaya ya Liwale mawasiliano ya simu ni kichocheo kikubwa cha kudumaza maendeleo yao.

11. MHESHIMIWA WEJJA (VITI MAALUM): Atamwuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: Kwa kuwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Dar es Salaam umezungushiwa uwigo sehemu yote ya kusini mwa kiwanja hicho kuonyesha mwisho wa kiwanja chenyewe; na kwa kuwa JWTZ Air Wing nao wamezungusha uwigo kuonyesha mwisho wa eneo hilo:

    (a) Je, Wizara kwa nini isiwaruhusu wananchi wanaoishi eneo la Ukonga sehemu ya Kipunguni kufanya maendeleo ya makazi yao;

    (b) Je, ni kwa nini Wizara inasita kuachia sehemu hiyo kwa wananchi wa Kipunguni ili iwe sehemu yao ya makazi ya kudumu;

    (c) Kama haiwezekani kuachiwa ni lini basi Wizara itakuwa wazi kwa wananchi hao.

WIZARA YA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:

12. MHESHIMIWA MAGANI (RUANGWA): Atamwuliza Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya

Juu: Kwa kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kupitia Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu; Wizara ya Elimu na Utamaduni na hata Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa imekuwa ikipata misaada ya nafasi za masomo katika fani mbalimbali kutoka nchi marafiki:

(a) Je, Serikali ilipata nafasi ngapi za masomo ya juu (Post graduate) kuanzia mwaka 1995 hadi hivi sasa, na ni nchi zipi ambazo zimetoa nafasi hizo;

(b) Je, katika nafasi zilizotolewa, Serikali ilitumia nafasi ngapi katika hizo;

(c) Je, Serikali ina utaratibu gani wa kupata wanafunzi wa kujaza nafasi hizo.

WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, WANAWAKE NA WATOTO:

13. MHESHIMIWA MKANGA (VITI MAALUM): Atamwuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto: Kwa kuwa kuna mikopo kwa ajili ya kuwawezesha wanawake kuendeleza miradi ili waweze kujikwamua kutoka kwenye dimbwi la umaskini;

Je, ni wanawake wangapi wenye ulemavu wamepatiwa mikopo hiyo nchini kwa kipindi cha mwaka 2000 mpaka 2001.

WIZARA YA FEDHA:

14. MHESHIMIWA ABDULLATIF HUSSEIN ESMAIL (MJI MKONGWE): Atamwuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha: Kwa kuwa TRA imesema kwamba imewafukuza wafanyakazi wake 1,492 kati ya 1992 hadi 2001 kwa tuhuma za rushwa na kutokana na kilio cha wananchi kwamba wanatumia mabavu na purukushani nyingi katika kutoza kodi:

(a) Je, nafasi zilizobaki wazi wameajiriwa wafanyakazi wengine;

(b) Je, TRA haioni kwamba yenyewe kuwachunguza wafanyakazi wake kuhusika na rushwa, kunawafanya wafanye kazi katika hali isiyo ya kawaida ya wasiwasi.

15. MHESHIMIWA NGWATURA (MBINGA MASHARIKI): Atamwuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha: Kwa kuwa baada ya kubinafsisha huduma za fedha, benki zote zimeelekeza huduma zake zaidi mijini na hivyo kuacha sehemu za mashambani bila huduma hiyo ya msingi, kwa maendeleo ya kiuchumi pamoja na mfumo mzima wa kijamii; na kwa kuwa athari za hali hiyo ni kuirudisha nchi kwenye biashara ya ujima (barter trade).

Je, Serikali inachukua hatua gani za kuhakikisha kuwa huduma za fedha zinasambazwa Vijijini pamoja na kuhakikisha mzunguko wa fedha (currency circulation) katika maeneo ya uzalishaji unakuwa endelevu badala ya kuwa wa msimu tu.

V. KAULI ZA MAWAZIRI

WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI

DODOMA **K.M.M.**
29 JANUARI, 2002 **KATIBU WA BUNGE**